

Kuishi Maisha Yanayompendeza Mungu (Sehemu ya 3)

Inategemea sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, KUJITAHIDI KUMPENDEZA MUNGU KUNA FAIDA?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Kwa nini huenda watu wengine wakasema hapana?

Kwa nini huenda wengine wakasema ndiyo?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

Matakwa ya Yehova yanatunufaisha naye hadai mengi kuliko tunavyoweza kutimiza.

(Ona sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 17-19.)

Soma Isaya 48:17, 18.

Ni kwa njia gani matakwa ya Yehova yanatunufaisha?

Soma Kumbukumbu la Torati 30:11-14 na Zaburi 103:14.

Mistari hiyo inaonyeshaje kwamba Yehova hadai tufanye mambo yanayopita uwezo wetu?



Tunapaswa kuvua utu wa zamani na kujivika utu mpya kama tu tunavyovua nguo chafu na kuvaa nguo safi

Tunapaswa kujitahidi kadiri tuwezavyo kuishi maisha yanayompendeza Mungu.

(Ona sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 20-22.)

Soma Waroma 12:9.

Kwa nini haitoshi tu kuepuka kufanya mambo ambayo Yehova anachukia?

Soma Wakolosai 3:9, 10.

Zaidi ya kuvua “utu wa zamani,” tunapaswa kufanya nini kingine ili kumpendeza Mungu?

Umefaidikaje kwa kuvaa “utu mpya”?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA...

Haiwezekani kubadili utu wako.

UNAWEZA KUSEMA HIVI...

Huenda watu wengi wanaamini hivyo. Lakini mimi siamini hivyo kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?

MTU AKISEMA...

Sheria za Mungu zinatunyima uhuru.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI...

Ni kweli kwamba Mungu ametupa sheria ili kudhibiti mwenendo wetu. Lakini ninaamini kwamba sheria hizo zinatunufaisha kwa sababu ...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?
